MWONGOZO KWA WATEJA

Mteja anaweza kuiomba Benki kuidhinisha kutoa fedha kwenye Akaunti kwa hundi zote, maelekezo ya kibenki, bili za kibiashara, hundi za amana, dhamana za mteja, dhamana za makubaliano ya kibenki au maelekezo mengine ya kibenki yatakayofanywa na Mteja mwenyewe au mwakilishi wake hata kama makato au utoaji wa fedha kwenye Akaunti yake utasababisha fedha kuondolewa kwa kiasi cha ziada (yaani Overdraft) au kwa kiwango kilichokubalika na Benki kulingana na huduma anazonufaika nazo.

Kama hakutakuwa na makubaliano ya kutolewa fedha za ziada katika Akaunti au kiwango chochote kisichokubalika na Benki, Benki itakataa kutoa fedha. Pia kama fedha zitakazoombwa na Mteja kwa ajili ya huduma hizi zitakuwa kubwa kuliko zilizokubaliwa na kuidhinishwa na Benki Mteja hatastahili kupewa.

Maelekezo ya Maombi yatakayotolewa na Mteja kwa Benki lazima yawekwe kwenye maandishi. Benki ina haki ya kujibu maelekezo hayo itakavyoona ni sahihi na itatumia aina yoyote ya mawasiliano na Mteja kulingana na hali ya uhusiano na Mteja na maelezo yake.

Benki kwa ridhaa yake yenyewe inaweza ikaruhusu maelekezo ya maombi kwa njia ya mawasiliano ya maandishi, kwa simu au mtandao wa kompyuta, lakini ina haki ya kusimamisha mawasiliano hayo na Mteja mpaka itakapopokea dhamana kutoka kwa Mteja au uthibitisho wa maandishi kwamba Benki itaendelea kushughulikia mawasiliano hayo na haitaathirika kutokana na hasara, gharama na athiri zozote zitakazotokea.

Iwapo tu Benki itawajibika kimkataba, Mteja anaweza kusimamisha mawasiliano na Benki kuhusu kutoa maelekezo ya maombi kwa hoja zitakazokubalika na Meneja wa Benki. Vinginevyo Benki itamtoza Mteja gharama zitokanazo na kusimamishwa kwa mawasiliano hayo kulingana na gharama zitakazowekwa na Benki.

Katika matukio yote yaliyoelezwa hapo juu, nguvu za kisheria za maelekezo ya mteja ni muhimu sana kwa Benki kuchukua hatua.

Benki ina haki ya kufunga au kusimamisha Akaunti bila kutoa taarifa kwa Mteja kama Benki itaona kuna tuhuma za maelezo ya ulaghai au yenye lengo la kukiuka sheria au kuiingiza Benki kwenye hasara.

UWEKAJI WA HUNDI NA MALIPO KWA NJIA YA HUNDI

Hundi zote na malipo ya aina yoyote ya kibenki yatawekwa au kutolewa kwa tahadhari za hasara au upotevu wa mali kwa Mteja mwenyewe, hata kama ilihusika kutuma hundi au kuchagua msafirishaji au wakala kwa hiyo. Kama malipo kupitia njia hiyo hayakufanyika na kusababisha hasara au upotevu wa mali, Benki itaondoa fedha kwenye Akaunti ya Mteja na kutoza riba. Ikiwa kama Benki imetoa fedha zaidi ya kiwango kulingana na utaratibu basi Mteja atalipwa fedha hizo.

Iwapo hundi au njia nyingine ya malipo ya kibenki itafanywa kwa ajili ya kutunisha Akaunti ya Mteja, Mteja ataruhusiwa tu kutoa fedha hizo iwapo Benki itaridhika zimekwisha kukusanywa na kuingia kwenye Akaunti.

Hata kama Mteja amepewa mkopo kupitia hundi, hawezi kuchukua fedha hadi hapo Benki itakapopata fedha kwenye kupitia njia ya hundi. Kama Mteja atalipwa kabla ya hundi kukusanywa au hundi ikionekana ni hewa Benki itatoa fedha hizo kwenye Akaunti au itatumia njia nyingine inayofaa pamoja na kutoza karo au riba.

Malipo yoyote yaliyolipwa kwa Mteja na kisha kubatilishwa lazima yarudishwe mara moja pamoja na riba inayostahili. Na Benki itakuwa na haki ya kukata fedha hizo au kuirejesha pamoja na riba kwa njia nyingine yoyote.

ADA ZA BENKI NA GHARAMA NYINGINE ZA HUDUMA

Mteja anatakiwa kukubali kuwa Benki ina haki ya kumtoza gharama za huduma, karo, riba, kodi au gharama nyingine zitokanazo na shughuli za kibenki kati ya Mteja na Benki. Mteja atawajibika kulipa ambapo Benki itatoa fedha kwenye Akaunti ya Mteja ikiwa ni pamoja na:-

Huduma za kisheria zikiwemo kukodi wanasheria, na gharama kwa Mteja zilizogharimiwa na Benki kupata huduma za kisheria au huduma zingine za kitaalamu au ushauri wa kitaalamu.

Iwapo tu itakubalika kwa maandishi riba kutozwa kutokana na uchukuaji fedha za ziada kwenye Akaunti, Benki itaamua kiwango cha makato wakati wowote ule. Riba itatozwa kila siku na malimbikizo yatakatwa kila mwezi. Benki haitamjulisha Mteja kiwango cha makato na riba. Riba itaendelea kukatwa mpaka kiwango cha makato kitakapokamilika bila kujali aina ya uhusiano wa Mteja na Benki.

Makato ya karo za huduma yatatozwa kwa viwango tofauti kulingana na aina za Akaunti na huduma zinazotolewa.

Mbali na hayo yaliyotajwa hapo juu, gharama nyingine ni karo ya hesabu za kibenki, utafutaji wa kumbukumbu, utoaji wa vitabu vya hundi, gharama za simu, kodi, gharama za uendeshaji wa Akaunti na zitokanazo na maombi ya Mteja.

Baada ya kusaini Masharti haya Mteja atakubali kuwa gharama hizi zinaweza kubadilika kulingana na mazingira ya shughuli za kibenki wakati huo. Hivyo basi Mteja anaidhinisha kuwa Benki inaweza kutoza makato ya aina zote au baadhi yaliyotajwa hapo juu bila kujulishwa kwa maandishi.

TAARIFA ZA KIBENKI

Mteja atalazimika kuangalia viashiria vyote vya hesabu katika taarifa yake ya Akaunti itakayotumwa na Benki. Kushindwa kufanya hivyo kwa kipindi cha siku 14 tangu kutumwa kwa taarifa hizo itaonekana kuwa Mteja ameridhika na kuidhinisha taarifa hizo. Hivyo Mteja hata kuwa na haki ya kuwasilisha madai kuwa kulikuwa na wizi, takwimu kutokuwa sahihi na madai mengine kutosikilizwa

MALALAMIKO YA MTEJA

Benki haitahusika kwa malalamiko yoyote kutoka kwa Mteja iwapo tu atawasilisha malalamiko hayo siku 7 baada ya tukio au jambo hilo. Kama malalamiko yamewasilishwa kwa muda huo na hayakufanyiwa kazi basi Mteja apeleke malalamiko tena haraka ili benki ichukue hatua.

BENKI HAIWAJIBIKI KWA MALALAMIKO

Benki haiwajibiki kwa hasara au uharibifu wowote utakaomuathiri yeyote katika mkataba huu ikiwa kama malipo ya bili kulingana na hasara hizo hayataarifiwa. Hata hivyo Benki itachukua hatua muhimu kuona kuwa madai yanashughulikiwa, hususani inapokea taarifa zake kutoka kwa Mteja kwa muda muafaka, hasa saa 24 ya kushughulikia bili hizo.

MALIPO YA FEDHA ZA ZIADA ZILIZOCHUKULIWA KWENYE AKAUNTI

Benki haitamruhusu Mteja kuchukua fedha zaidi ya kiwango cha kima cha chini cha akiba. Pia Mteja hataruhusiwa kuchukua fedha za malipo ya ziada ya Benki kinyume na kiwango kilichokubaliwa na kuidhinishwa na Benki katika utoaji wa huduma hiyo.

Ikiwa kama Mteja amechukua fedha kutoka kwenye Akaunti zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa au kiwango cha chini cha akiba cha malipo ya ziada kilichoidhinishwa basi Benki itamtoza karo pamoja na malimbikizo ya riba.

Mteja atalazimika kulipa gharama kutokana na kuchukua zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa kibenki pamoja na riba au karo nyingine zinazotozwa na Benki.

HAKI YA KUHAMISHA FEDHA KWENDA KWENYE AKAUNTI YENYE MADENI

Benki kwa wakati wowote ule ina haki ya kuhamisha fedha kutoka kwenye Akaunti moja ya Mteja kwenda kwenye akaunti nyingine ya Mteja huyo ili kufuta madeni na hii itahusisha:-

(i) *Akaunti ya aina yoyote ya mkopo, akaunti ya amana, akiba au za kikundi cha amana.*

(ii) *Muda wowote hata kama akaunti maalum ya akiba haijakomaa.*

Kwa taarifa Benki itakata fedha katika Akaunti nyingine ya Mteja huyo ili kufuta madeni katika akaunti nyingine bila kujali kuwa Mteja huyo anadaiwa na mwingine.

Kama Mteja atahusika kwenye akaunti nyingine yenye fedha kama Mdhamini basi akaunti hiyo itahusika kulipa madeni yaliyolimbikizwa kwenye akaunti ya Mteja huyo.

HAKI YA KUDAI MALI ZISIZOHAMISHIKA NA NYINGINE

Wakati Mteja anadaiwa Benki ina haki ya kuchukua au kufilisi mali zisizohamishika au zinazohamishika za Mteja kama vile eneo la ardhi iliyoendelezwa, nyumba, mashine, gari, madini yaliyo hifadhiwa yenye thamani, umiliki wa migodi na nyingine ili kulipa madeni.

Mali zilizowekwa na mteja Benki kwa ajili ya hifadhi maalum zitatumika pia kulipa madeni ya Mteja huyo.

Kama Mteja ameidhinisha Benki kutumia mali zake kwa ajili ya kulipa madeni basi Benki itafanya hivyo ili kufuta madeni na Mteja huyo hataruhusiwa kutumia mali hizo.

Ikiwa kama Benki imetoa taarifa na Mteja hajatoa majibu yoyote baada ya siku 14 Benki itatumia mali za Mteja huyo zilizowekwa kama dhamana au hifadhi ya ulinzi wa mali, kulipa madeni yote ya Mteja huyo.

Kama deni halijalipwa kwa muda uliotajwa Mteja atashirikiana na Benki ili mali zake zilipie madeni na salio lake litawekwa kwenye Akaunti ya Mteja.

Benki haitahusika na matokeo yoyote ya zoezi hili, itahusika endapo tu itabainika Benki imefanya hivyo kwa ulaghai.

Akaunti ya Mteja ya fedha za kigeni itahusika pia kulipia madeni kwenye akaunti zingine za mteja zenye madeni. Thamani ya fedha hizo italingana na bei ya fedha za kigeni ya tarehe iliyohusika na zoezi hilo. Benki haitahusika na hasara yoyote itokanayo na ubadilishaji wa fedha hizo za kigeni

Amana zilizowekwa kwa muda maalum zikiwemo za fedha za kigeni zitatumika pia kulipia madeni hata kama amana hizo zimepitwa na wakati au hazijafikia muda wa kukomaa.

KUFUTA AKAUNTI

Benki inaweza kufuta Akaunti ya Mteja ikiwa kama itabainika kuwa kuna mgogoro katika umilikaji wa akaunti na Benki inaona ni muhimu kuifuta ili isiwajibike. Benki itafanya hivyo tu ikiwa na uhakika kuwa maamuzi hayo hayataiwajibisha kisheria kudaiwa fidia au madai mengine yoyote.

VITABU VYA HUNDI

Vitabu vya hundi hutolewa kwa masharti yafuatayo:-

- *Mteja atatumia hundi na kuhifadhi vitabu kwa uangalifu wa hali ya juu.*
- *Mteja anakubali kuhakikisha kuwa:-*

Fomu za hundi zinahifadhiwa mahali penye usalama

Kwamba Benki inataarifiwa haraka ikiwa kama Mteja amebaini kuwa kitabu cha hundi kimeibiwa au kimepotea.

Mtu aliyeidhinishwa kuandaa hundi kwa niaba ya Mteja anafanya hivyo.

Hundi zinasainiwa kwa wino mzuri usioweza kufutika.

Kiasi cha fedha kitakachoandikwa kinajazwa ipasavyo sehemu ya kushoto bila kuruhusu tarakimu nyingine za kughushi. Hundi yoyote isiyokamilishwa kujazwa isitolewe kwa mtu mwingine asiyehusika.

Mwenye haki ya kusaini:
Hundi na mabadiliko yanayoambatana nayo yasainiwe na mtu aliyeidhinishwa kuwa muweka sahihi.
Hundi yoyote ambayo haijakamilika isikabidhiwe kwa mtu asiyetambulika au mtu mwingine asiyeaminiwa na mteja.

- *Mteja anashariwa kuwa:-*

Ni muhimu kuifunga hundi (crossed cheque) ili itumike tu kwa idhini ya Benki

Ikiwa kama inajulikana kuwa anayetumia anajulikana na Benki anayotumia basi ni muhimu kuandika jina la Benki kwenye hundi iliyofungwa.

Benki ikipokea hundi ambayo imeelekezwa kuwa malipo yasimamishwe, Benki itafanya hivyo.
Benki itanakili namba ya hundi na vielelezo vingine na haitahusika na malalamiko yatokayotolewa.

Wakati akaunti inafungwa Mteja atarudisha vitabu vya hundi

Benki ina haki ya kuikataa hundi ambayo haijakidhi masharti na matakwa yaliyokubalika katika mkataba huu.

UCHUKUAJI WA FEDHA TASLIMU

Benki itawajibika kulipa pesa taslimu iwapo tu hundi itasainiwa na muwekaji au wawekaji sahihi wanaotambuliwa. Pia hundi inatakiwa iambatanishwe na barua ya Mteja.

Iwapo malipo ya fedha taslimu hayatamhusisha Mteja bali mtu mwingine asiyetambuliwa na Benki, basi Mteja au mwakilishi wake anapaswa kumtambulisha anayestahili kulipwa.

Utambulisho unaweza kuwa kwa njia ya simu au nyingine kabla ya Benki kulipa.

Iwapo malipo ya fedha taslimu kupitia hundi yatawasilishwa na waajiriwa au mwakilishi anayefahamika na Mteja yafuatayo yatafanyika:-

Mwajiriwa atatambuliwa kwa utaratibu ambao Benki imeweka.

Kikomo cha malipo lazima kikubalike kwa muafaka kati ya Mteja na Benki la sivyo Benki haitalipa.

Wakati malipo yanafanyika kwa kufuata kifungu cha maelekezo hapo juu katika kifungu hiki, Mteja lazima aweke dhamana dhidi ya hasara itokanayo na malipo hayo yatakayomnufaisha yeye, mwakilishi wake, au mtu mwingine yeyote.

Iwapo mwajiriwa au mwakilishi wa Mteja hatafahamika na Benki au malipo yamezidi kikomo cha kiwango basi kifungu cha maneno ya hapo juu kitatumika ikiwa na maana kuwa mwajiriwa au mwakilishi atafahamika ni mtu wa tatu katika mkataba.

- *Mtu mwingine aliyekasimiwa na Benki*

Kwa mujibu wa sheria za nchi na iwapo Mteja amekubali pia iko ndani ya utaratibu wa kibenki.

MUDA WA KUKAMILISHA HESABU

Muda wa kukamilisha hesabu za Mteja utatokana na ridhaa ya Benki. Muda unaweza kuwa kila mwezi, kila robo mwaka, nusu mwaka au kila mwaka.

AKAUNTI ZA WATOTO

Kwa Akaunti zote za watoto ambazo zitafunguliwa na wazazi na walezi, Benki itaomba idhini ya wazazi au walezi kwa kuendesha Akaunti za Watoto, hadi hapo benki itakapojulishwa kwa maandishi na wazazi au walezi kwa mabadiliko yatakayofanywa.

KUKASIMU KAZI ZA BENKI

Benki inaweza ikakasimisha au kuhamisha haki na kazi au wajibu wake kwa mtu mwingine kulingana na vigezo na masharti haya. Inaweza kufanya hivyo bila kutoa taarifa kwa Mteja.

KUFUNGA UHUSIANO WA KIBIASHARA

Benki inaweza kurekebisha au kusimamisha uhusiano wa kibiashara na mteja muda wowote bila kutoa taarifa. Inaweza kusimamisha mkopo kwa ridhaa yake yenyewe.

UTOAJI TAARIFA KWA MTEJA

Taarifa zozote, barua au mawasiliano yatatolewa kwa kutumia kumbukumbu za mwisho za mahali Mteja alipo.

Mawasiliano na Mteja yatakuwa yamefanywa kwa kutumia njia zifuatazo:-

Kusafirisha kwa mkono

Mawasiliano kwa njia za simu za maneno, maandishi ya teleksii au faksi na maandishi kwa njia ya mtandao wa kompyuta ambapo yatatakiwa yafanyike siku za kazi.

Kwa njia ya posta yakamilike baada ya siku 7 za kazi zinazofahamika hapa Tanzania. Pia barua inatakiwa iwe na stempu na muhuri wa posta.

Mteja hana haki ya kuidai Benki ikiwa kama mawasiliano hayo yamevurugika au yameharibika.

MAREKEBISHO YA VIGEZO NA MASHARTI YATUMIKAYO KATIKA AKAUNTI

Benki ina haki ya kufanya marekebisho ya vigezo na masharti haya na itamjulisha Mteja kwa njia ya mawasiliano ya barua au kwenye sehemu ya ubao wa matangazo unaoweza kufikiwa na watu wengi.

NGUVU YA KISHERIA

Benki haitawajibika kutochukua hatua kwa mteja atakayekiuka mkataba huu bali itaendelea kuchukua hatua muhimu kulingana na masharti na matakwa ya mkataba isipokuwa pale tu sababu za ukiukaji ni kwa mambo yasiyozuilika kama vile amri za kiserikali, vita, gharika, matetemeko ya ardhi, dhoruba na majanga mengine asilia.

SHERIA NA MAMLAKA

Masharti na Matakwa haya ya kuendesha akaunti yanalingana na kutii sheria za Tanzania na Mteja anaweza akapewa au akanyimwa haki mbele ya mahakama za Tanzania.

Pamoja na hayo yaliyoainishwa hapo juu, Benki inaweza kufungua mashtaka Mahakamani dhidi ya Mteja kwa ridhaa yake bila kuzuiliwa na chombo au mtu yeyote.